



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA
HALMASHAURI YA WILAYA YA RUNGWE



Tarehe: 03/03/2022

TANGAZO LA MNADA WA HADHARA

1. Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Rungwe anawatangazia wananchi, wafanyabiashara, makampuni mbalimbali juu ya mnada wa hadhara. Kwa idhini tuliyopewa na Katibu Mkuu Hazina, tunakusudia kufanya mnada wa hadhara wa mali chakavu (Mali zilizotumika) kama vile magari, pikipiki, jenereta, vifaa vya ofisi, vifaa vya Hospitali n.k siku ya tarehe 17 -18/03/2022 kuanzia saa 4:00 asubuhi katika viwanja vya Jengo la zamani la Ujenzi mtaa wa Mabonde na Hospitali ya Wilaya Tukuyu (Makandana) na kwamba baadhi ya mali hizo zimeorodheshwa kwenye jedwali hapa chini:-

S/N	Aina ya mali/	Mahali zilipo	Namba ya Usajili
1	Isuzu TX Lorry Truck	Idara ya ujenzi zamani	SM 85
2	Isuzu Tipper Truck	Idara ya ujenzi zamani	SM 1301
3	Toyota Land cruiser P/up	Idara ya ujenzi zamani	STH 1130
4	Land Rover 109	Shule ya Sekondari Rungwe	STG 9983
5	Motor Cycle Honda 110	Halmashauri ya Wilaya	STH 1130
6	Motor Cycle Non Fang	Halmashauri ya Wilaya	STH 8855
7	Tri - Motor cycle SUNLG-GUTA	Halmashauri ya Wilaya	SM 12173
8	Tri - Motor cycle SUNLG-GUTA	Halmashauri ya Wilaya	SM 12174
9	Vifaa vya Hospitali n.k	Hospitali ya Tukuyu	

Masharti ya Mnada

- i. Mnunuzi anatakiwa kulipa fedha 25% ya bei ya thamani ya mali iliyonunuliwa siku ya mnada na kiasi kilichobaki kitatakiwa kulipwa ndani ya siku saba (7) na kwamba kinyume na hapo kiasi kilichotolewa hakitarudishwa kwa mnunuzi na kwamba mnada utarudiwa tena.
- ii. Ukaguzi wa mali husika utafanyika kabla ya siku ya mnada tokea tarehe ya tangazo kuanzia saa 4:00 asubuhi hadi saa 8:00 mchana, siku ya kazi..
- iii. Gharama za kubadilisha umiliki (Transfer of ownership), kodirna gharama nyingine zote zitakuwa ni jukumu la Mnunuzi.
- iv. Mali itauzwa kama ilivyo na mahali ilipo.
- v. Mnunuzi atawajibika kuondoa/kuchukua mali aliyonunua ndani ya siku saba(7) kuanzia siku ya kukamilisha malipo.
- vi. Mnada usipofikia thamani halisi ya mali husika utahairishwa.

2. Imetolewa na,

Mchau, R.B

MKURUGENZI MTENDAJI (W)
HALMASHAURI YA WILAYA YA RUNGWE

MKURUGENZI MTENDAJI (W)
RUNGWE